STRIVE
Tackling the structural drivers of HIV

MITU
Mwanza Intervention Trials Unit

# Maisha: Mikopo midogomidogo na mafunzo ya kijinsia kwa ajili ya kupunguza ukatili dhidi ya wanawake

Sasa linatambuliwa kama tatizo kubwa kwa afya ya jamii na maendeleo ulimwenguni kote, ukatili unaofanywa na wenzi unasababisha maumivu, kuwashushia hadhi wanawake na unashadidia mfumo dume, unavunja sheria za nchi na unahusishwa na kuongezeka hatari za maambukizi ya UKIMWI. Ushahidi zaidi unahitajika kuhusiana na njia bora ya kuzuia na kupunguza ukatili huu.

## MAISHA NI NINI?

Utafiti wa Maisha unatathmini afua zinazosaidia kujenga mahusiano yenye afya, yasiyokuwa na ukatili kutoka kwa mwenza. Unafanya haya kwa kuwajengea uwezo wanawake kiuchumi na kijamii kupitia mikopo midogomidogo na mafunzo ya kijinsia. Utafiti wa Maisha unapima iwapo vitu hivi vinafanya kazi katika kupunguza unyanyasaji wa wanawake toka wenzi wao, kichochezi cha kimfumo cha maambukizi ya UKIMWI.

**Je mafunzo ya jinsia, ama pekee au pamoja na upatikanaji wa mikopo midogomidogo inaweza kupunguza kiwango cha unyanyasaji dhidi ya wanawanawaketoka mwenza wao?**

**Utafiti wa Maisha umebuniwa kupata jawabu:**
Kitengo cha tafiti za magonjwa ya binadamu (MITU) kinafanya kazi na matawi ya shirika lisilokuwa la kiserikali (NGO) linalotoa mikopo midogomidogo Bangladesh Rural Advancement Committee (BRAC) katika kutekeleza utafiti wa Maisha Mwanza, Kaskazini mwa Tanzania. Mradi unafanyika kuanzia 2014 hadi 2019. MITU na London School of Hygiene & Tropical Medicine (LSHTM) (Chuo Kikuu cha London cha Afya na Magonjwa kaatika nchi za joto) wanaratibu utafiti wa pamoja wa STRIVE unaofadhiliwa na Department for International Development (DFID) (Idara ya serikali ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa). Maisha unahusisha makundi mawili yaliwekwa kwa Bahati nasibu yanathibitiwa pamoja na mbinu ya nyongeza za utafiti wa ubora na mchakato husishi wa tathmini na ukadiriaji gharama kiuchumi.

## MSINGI

Utafiti wa Maisha unajenga katika yaliyoonekana kwenye afua ya utafiti wa mikopo midogomidogo kwa UKIMWI na stahili kijinsia (IMAGE) iliyofanyika kwenye maeneo ya vijijini nchini Afrika Kusini. IMAGE iliunganisha mikopo midogomidogo kupitia mtaala wa mafunzo shirikishi ya kijinsia na UKIMWI yaliyotolewa kwa washiriki waliokuwa katika vikundi vya mikopo. Utafiti uliohusisha makundi mawili yaliyowekwa kwa Bahati nasibu na kuthibitiwa uligundua kuwa, kwa zaidi ya kipindi cha miaka miwili, IMAGE ilipunguza kwa 55% matukio ya ukatili wa kijinsia kutoka kwa wenza miongoni wa washiriki wa utafiti.

**Utafiti pia uligundua kuwa IMAGE:**

* ilipunguza kwa kiasi kikubwa umaskini wa kaya
* Ilijenga uwezo wa washiriki (kama ulivyoonyeshwa na hali ya kujiamini zaidi, uwezo huru wa kufanya maamuzi, na kuongeza uwezo wa kukabili miiko ya kijinsia)
* iliongeza mawasiliano ndani ya familia kuhusiana na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI
* iliongeza taarifa za matumizi ya kondomu miongoni mwa washiriki vijana katika mahusiano nje ya ndoa
* iliongeza uwezekano kuwa washiriki vijana wangeweza kupimwa virusi vya UKIMWI

**Kuna maswali yamebaki baada ya IMAGE na Maisha imebuniwa ili kuyajibu:**

* Yale mabadiliko yalitokana na mikopo midogomidogo au mafunzo ya kijinsia?
* Utaratibu huu unaweza kufanikiwa kwenye maeneo mengine ya Afrika kusini mwa Sahara?

## TATHMINI

Utafiti wa Maisha unakusudia kujibu mlolongo wa maswali:

* Kuunganisha mikopo midogomidogo na mafunzo ya jinsia kunaweza kufanikisha kupunguza ukatili wa kijinsia kutoka kwa wenza nchini Tanzania?
* Je upunguzaji kama huu wa matukio ya ukatili wa kijinsia unaofanywa na wenza unaweza kupatikana pia kwa kutoa mafunzo ya jinsia kwa wanawake kwa wasiopata mikopo midogomidogo?
* Ni njia zipi mwafaka za kupunguza ukatili wa kijinsia unaotendwa na wenza na jinsi gani ya utafiti unaziongezea ubora?
* Je mikakati hii inatekelezeka (gharama zake zinachukulika)?



# Sehemu mbili za

**SEHEMU A (JARINIO LA KWANZA)**

66 VIKUNDI VILIVYOKUWEPO VYA MIKOPO MIDOGOMIDOGO

Kila kikundi kinaundwa na wastani wa wanawake 15. Makundi haya tayari yanapokea mikopo midogo midogo kutoka mashirika husika ya huduma hizo ya BRAC. tayari yanapokea mikopo midogo midogo kutoka mashirika husika ya huduma hizo ya BRAC. Mchakato wa kuyapanga kwa Bahati nasibu utatumika ili kutambua ni makundi yapi yatapata mafunzo ya jinsia kabisa na yapi yatapata.Wawakilishi wa makundi wanashiriki katika mchakato huu wa kuyapanga makundi.

## A1

**Makundi 33 yanapata mikopo midogomidogo pekee**

A1 ni kundi lisilopata mafunzo. Wanawake katika makundi haya wanaendelea kukopa fedha na kushiriki katika shughuli za kila wiki za BRAC kama walivyokuwa wakifanya tangu mwanzo. Hawapati mafunzo ya kijinsia katika kipindi cha utafiti wa Maisha.

## A2

**Makundi 33 yanapata mikopo midogomidogo na mafunzo ya jinsia**

Wanawake katika makundi haya wanaendelea kukopa fedha na kushiriki katika shughuli za kila wiki za BRAC kama walivyokuwa wakifanya tangu mwanzo. Kwa nyongeza wanashiriki katika vipindi 10 vya mafunzo ya jinsia. Vipindi hivi vimetengenezwa na taasisi ya EngenderHealth na vinatokana na mitaala iliyopo ikiwa na pamoja na Sisters for Life ambayo ni sehemu ya IMAGE. Vipindi hivi vinafanyika kila baada ya wiki mbili wakati vikundi vinafanya vikao vya marejesho ya mikopo. Wawezeshaji wawili wa mafunzo ya jinsia wanaongoza mafunzo kila kipindi.

Utafiti unalinganisha kiwango cha ukatili wa kijinsia unaosababishwa wa wenza ndani ya A1 na ndani ya A2 katika mwaka wa pili. Je ukatili umepungua ndani ya mahusiano ya wanawake walioshiriki mafunzo ya jinsia pamoja na mikopo midogomidogo?

### Matokeo kwa wanawake na familia zao

Utafiti wa Maisha unapima:

* wanawake walioripoti kuwa wamefanyiwa ukatili kimwili na/au kingono miaka miwili baada ya kushiriki kwenye utafiti
* tija ya kikundi cha mikopo (kwa sehemu ya mikopo midogomidogo)
* umiliki wa vitu ndani ya nyumba
* uwiano wa mawasiliano ndani ya nyumba na usuluhishi wa migogoro
* afya ya uzazi na kujamiiana, pamoja taarifa za tabia kingono na utumiaji wa huduma
* kuongeza kwa matatizo ya kiakili
* uwezo wa kuhimili shinikizo za kijamii na kupinga za mila potofu

## Ni jitihada zipi zina ufanisi zaidi dhidi ya ukatili wa kijinsia unaofanywa na wenza:

**A1:** mikopo midogomidogo pekee?

**A2:** mikopo midogomidogo pamoja na mafunzo ya jinsia?

**B2:** mafunzo ya jinsia pekee?

# utafiti wa Maisha

## SEHEMU B (JARIBIO LA PILI)

### VIKUNDI VIPYA 66

Kila kikundi kinaundwa na wastani wa wanawake 15. Makundi haya mapya yameundwa na timu ya Maisha. Mchakato wa kuyapanga makundi kwa Bahati nasibu utatumika ili kutambua makundi yapi hayataapaata maafunzo ya jinsia kabisa na yapi yatapata. Wawakilishi wa makundi wanashiriki katika mchakaato huu wa kuyapanga makundi.

### B1

**Makundi 33 yasiyopata uwezeshaji wa aina yoyote**

B1 ni kundi la kulinganishia. Timu ya maisha inaendelza mawasiliano na wanawake kwenye makundi haya, lakini hakuna kitu chochote kitafanywa kwa wanawake hawa.

### B2

**Makundi 33 yatapata mafunzo ya jinsia bila mikopo midogomidogo**

Wanawake katika vikundi hivi watashiriki mafunzo kwenye vipindi 10 sawa na yaliyotolewa kwa A2. Vipindi hufanyika kila baada ya wiki mbili. Wawezeshaji wawili wataongoza kila kipindi.

Utafiti unalinganisha kiwango cha ukatili wa kijinsia unaofanywa na wenza ndani ya makundi ya B1 na B2 katika mwaka wa pili. Je ukatili umepungua mafunzo ya jinsia yaliyotolewa kwa wanawake wasipata mikopo midogomidogo yamepunguza ukatili wa kijinsia ndani mahusiano?





### Matokeo kwa wenza wa kiume

Utafiti kwa wenzi wa kiume wa wanawake wanaoshiriki katika sehemu A (Utafiti wa 1) unachunguza mitizamo ya wanaume kuhusiana na ukatili wa kijinsia unafanywa na wenzi na kama mafunzo ya jinsia yaliyotolewa kwa wanawake yana matokeo yeyote kwa wanawake:

* taarifa kufanyika kwa ukatili wa kijinsia uliofanywa na mwenzi
* mtazamo juu ya ukatili wa kijinsia baina ya wenzi
* uwezo wa kupinga shinikizo la kijamii na kupambana na mila potofu

## MATOKEO

Ni dhahiri kuwa ukatili wa kijinsia baina ya wenzi unawadhuru wanawake na mahusiano yao na familia zao. Unahusishwa na kuongezeka hatari ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na matatizo mengi ya kiafya. Gharama za ukatili wa kijinsia baina ya wenzi ni kubwa kwa serikali kadhalika kwa watu binafsi na familia. Kitu ambacho hakifamiki bado ni jinsi ya kuushughulikia; namna bora ya kuzuia ukatili wa kijinsia baina ya wenzi. Hii ndiyo thamani ya utafiti kama IMAGE na Maisha; zinaonyesha matokeo and gharama za afua mahsusi ya kupunguza ukatili baina ya wenzi. Kutokana na matokeo ya IMAGE, mikopo midogomidogo na uwezeshaji wa wanawake inajumuishwa rasmi katika mkakati wa serikali wa kupambana na virusi vya UKIMWI na UKIMWI nchini Afrika Kusini. Inatumainiwa kuwa tukayojifunza toka utafiti wa Maisha utasaidia pia kuelekeza sera, mipango na ugharimiaji unalenga kupunguza ukatili wa kijinsia baina ya wenzi na kuzalisha faida nyingi kwa mahusiano miongoni mwa watu, afya, ustawi wa kijamii.





### WATAFITI

**Dr Saidi Kapiga**, MITU

**Dr Gerry Mshana**, NIMR

**Dr Shelley Lees, Dr Sheila Harvey, Dr Christian Hansen and Prof Charlotte Watts**, LSHTM

### WADAU

Utafiti wa Maisha ni mradi wa ushirikiano wa kituo cha afya na ukatili wa kijinsia katika LSHTM na Taasisi ya taifa ya utafiti wa magonjwa ya binadamu (NIMR) Mwanza, kitengo cha utafiti (MITU). Taasisi hizi zinaleta kwa pamoja uzoefu wa ushirikiano na ujuzi wa pamoja katika kufanya tafiti kubwa za kijamii kama vile mikopo midogomidogo namipango ya kuzuia ukatili wa kijinsia.

### SHUKRANI

Utafiti wa Maisha unafadhiliwa na mipango ya utafiti wa pamoja wa STRIVE unaofadhiliwa na DFID. Hata hivyo, maoni yalitolewa si lazima yaakisi sera za idara. Mfadhili asiyependa kutambuliwa ametoa ufadhili wa nyongeza.

### REJEA

World Health Organization/London School of Hygiene & Tropical Medicine. *Preventing intimate partner and sexual violence against women: Taking action and generating evidence*. Geneva; 2010

Pronyk PM, Hargreaves JR, Kim JC, Morison LA, Phetla G, Watts C, et al. Effect of a structural intervention for the prevention of intimate-partner violence and HIV in rural South Africa: a cluster randomised trial. *The Lancet*. 2006; 368(9551): 1973-83

Kim J, Ferrari G, Abramsky T, Watts C, Hargreaves J, Morison L, et al. Assessing the incremental effects of combining economic and health interventions: the IMAGE study in South Africa. *Bull World Health Organ*. 2009; 87(11): 824-32

Pronyk PM, Kim JC, Abramsky T, Phetla G, Hargreaves JR, Morison LA, et al. A combined microfinance and training intervention can reduce HIV risk behaviour in young female participants. *AIDS*. 2008; 22(13): 1659-65

Jewkes R, Nduna M, Levin J, Jama N, Dunkle K, Puren A, et al. Impact of stepping stones on incidence of HIV and HSV-2 and sexual behaviour in rural South Africa: cluster randomised controlled trial. *BMJ*. 2008; 337: a506

Garcia-Moreno C, Jansen HA, Ellsberg M, Heise L, Watts CH, Health WHOM-cSoWs, et al. Prevalence of intimate partner violence: findings from the WHO multi-country study on women's health and domestic violence. *The Lancet*. 2006; 368(9543): 1260-9

Heise, L. *What works to prevent partner violence: An evidence overview*. STRIVE. London. 2011.

Kwa maelezo zaidi, Wasiliana na:

Timu ya Maisha | PO Box 11936 | Mwanza, Tanzania | T: 028-250 0019 | **www.mitu.or.tz**

http://strive.lshtm.ac.uk

STRIVE Tackling the structural drivers of HIV

MITU Mwanza Intervention Trials Unit

National Institute for Medical Research

UKaid from the British people

London School of Hygiene & Tropical Medicine